

# Tanzania Media Women's Association

CHAMA CHA WAANDISHI WA HABARI WANAWAKE TANZANIA

P.O BOX 741, Tunguu Zanzibar

Phone 0772378378/

Email: [info@tamwaznz.or.tz](mailto:info@tamwaznz.or.tz)



24 /11/2021

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### Siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia:

- Wadau wanasema ukatili kwa wanawake na watoto sasa basi.

Wakati dunia inaadhimisha siku 16 za harakati za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto , taasisi zisizo za kiserikali Zanzibar zinaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku hizo kwa kusositiza juu ya kuandaa mikakati ya pamoja ya kuhakikisha kwamba kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto zinashughulikiwa kwa haraka katika uchunguzi, kupelekwa mahakamani na kutolewa hukumu kwa mujibu wa sheria.

Taasisi hizo ni pamoja na Umoja wa Watu wenyе Ulemavu Zanzibar (UWZ), Kituo cha Huduma za Kisheria Zanzibar (ZLSC), Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA),Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Zanzibar Gender Coalition (ZGC), Umoja wa Wanawake wenyе Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Shirika la Kupambana na Changamoto za Vijana Zanzibar (ZAFAYCO), Mashirika ya Wasaidizi wa Kisheria Zanzibar (ZAPAO), Mtandao ya Kupinga Vitendo vya Udalilishaji Zanzibar, Kijiji cha Watoto SOS, Jumuiya ya Vijana na Elimu Kaskazini (JUVIEKA) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Zanzibar (TAMWA, ZNZ ).

Kauli mbiu ya taasisi hizo kwa mwaka huu ni “**Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto Basi**”. Kauli hii inakwenda sambamba na kauli mbiu ya kimataifa isemayo “Orange the world: End violence against women now!” {**Dunia ya amani: Maliza ukatili dhidi ya wanawake sasa**} na ile ya kitaifa isemayo “**Tuimarishe Amani Zanzibar: Tumalize vitendo vyta ukatili na udhalilishaji sasa**” kauli mbiu zote zinasisitiza juu ya umuhimu wa kuchukua hatua katika kumaliza kabisa vitendo vyta ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Wakati Siku 16 za kupinga vitendo vyta ukatili wa kijinsia zikiadhimishwa, bado kuna changamoto nyingi zinazowaandama wanawake na watoto vikiwemo vitendo vyta udhalilishaji na ukatili wa kijinsia na kutokuwepo mifumo mizuri ya kuwalinda na kuwapatia haki zao kwa wakati muafaka.

Kwa mujibu wa rikodi za TAMWA ZNZ tangu mwaka 2016, matukio 21 ya mauwaji ya wanawake na watoto yameripotiwa (wanawake 17 na watoto wanne) ambapo ni matukio machache tu ndiyo yaliyofikishwa katika Mahakama Kuu ya Zanzibar yakiwemo ya Wasila Mussa (21), Hajra Abdallah Abdallah (21) na samira Sultan Abdallah (56).

Mbali na matukio ya mauaji ya wanawake, pia jumla ya kesi 717 za udhalilishaji wa wanawake na watoto zimeripotiwa kuanzia Januari hadi Agosti, 2021. Kwa mujibu wa takwimu kutoka ofisi ya mtakwimu Mkuu wa Serikali, kati ya kesi hizo, 360 ni za ubakaji, kesi 50 kuingilia kinyume cha maumbile, kulawiti kesi 99, kesi 62 kutoroshwa, kesi 62 shambulio la aibu/kukashifu na kesi 84 ni za shambulio.

Katika kuadhimisha siku 16, wadau wamejipanga kuendelea kupaza sauti zao kukemea vitendo vyote vyta udhalilishaji kwa kutoa elimu juu ya athari ya vitendo vyta ukatili kwa wanawake na watoto kwa kutumia vyombo vyta habari, pamoja na kampeni maalum katika mitandao ya

kijamii, warsha na mafunzo mbalimbali kwa makundi maalum wakiwewmo watu wenye ulemavu.

Katika maadhimisho haya pia kutakuwa na makongamano mbalimbali yatakayowahusisha wanafunzi, taasisi za serikali na zisizo za kierikali zinazosimamia sheria, na jamii kwa ujumla ambapo pamoja na mambo mengine yataangalia mafanikio na changamoto katika mapambano dhidi ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Siku 16 za Kupinga Ukatili wa kijinsia ni kampeni maalumu ya kimataifa kufuatia mauaji ya kinyama ya wanawake wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominika mwaka 1960. Umoja wa Mataifa mwaka 1991 ilitangaza siku hizi 16 kendesha kampeni ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wanawake.

Maadhimisho haya huanza tarehe 25 Novemba na hufikia kilele tarehe 10 Desemba ambayo ni Siku ya Kimataifa ya Kuadhimisha Tamko Rasmi la Haki za Binadamu, ikiwa ni ishara ya kuhusisha ukatili dhidi ya wanawake na haki za binadamu na vile vile kutia msisitizo kwamba ukatili wowote wa kijinsia ni uvunjwaji wa haki za binadamu.

**Dkt, Mzuri Issa**

**Mkurugenzi,**

**TAMWA, ZNZ.**